**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Sita – Tarehe 24 Disemba, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

221. MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA (Jimbo la Shaurimoyo) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Ukuta unaozuia maji ya bahari uliopo mbele ya hoteli maarufu hapa Zanzibar Africa House umeanguka na kusababisha maji ya bahari kuingia hadi barabarani. Ukuta ule ni mrefu ambapo unahatarisha hata majengo yaliyopo karibu na jengo hilo ikiwemo Shirika la Nyumba hadi Ikulu ya Zanzibar Mnazi Mmoja. Kwa kuzingatia ukuta ule umejengwa tangu enzi ya ukoloni na haujawahi kufanyiwa ukarabati wa aina yoyote ile.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri suala hili unalijua.

(b) Na kama unalijua, Serikali kupitia Wizara yako ina mpango gani kabambe wa kuushughulikia ukuta huo.

(c) Na kama upo huo mpango, Je, tutegemee ukuta huo utakarabatiwa lini.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

162. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga jengo jipya la Mahakama Kuu Tunguu. Pamoja na pongezi hizo nachukuwa fursa hii kueleza masikitiko ya wananchi juu ya uchakavu wa Mahakama za Mkokotoni, Wete na Konde, hali ambayo inarudisha nyuma ufanisi wa kazi kwa watumishi wa Mahakama hizo.

(a) Kwa kuwa Mahakama hizo ni za muda mrefu na hazijafanyiwa ukarabati wowote Je, ni lini Serikali itaanza kuzifanyia ukarabati.

(b) Kwa kuwa Mahakama ya Mkokotoni iko katika hali mbaya Zaidi, Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika wa kusitisha matumizi ya Mahakama hiyo na kutafuta eneo jengine.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

29. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali inastahili kupongezwa kwa maelekezo yake kuhusu upatikanaji na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa na vitambulisho, vikiwemo vyeti vya kuzaliwa nje ya muda. Hata hivyo, kuna malalamiko kuwa masheha wengi waliomo ndani ya jimbo la Pandani huwakwamisha wananchi, hasa watu wenye miaka 18 na zaidi katika mchakato wa kutafuta vyeti.

(a) Je, hatua gani wananchi wanatakiwa kufuata pindi wakinyimwa haki yao ya msingi ya kupatiwa huduma ya vyeti vya kuzaliwa kama wanavyofanyiwa na wafanyakazi wa Wilaya ya Wete.

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kuwagundua na kuwahukumu wahusika wa vyeti feki na masheha wanalalamikiwa kuwanyima wananchi haki zao kwenye vyeti na vitambulisho.

(c) Je, Serikali haioni haja ya kutoa muongozo kuhusu uhusiano wa magamba halali ya kliniki na vyeti vya kuzaliwa.

93. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inachukua jitihada mbali mbali za kuhakikisha mji wetu unakuwa na mpangilio mzuri wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Licha ya jitihada hizo, bado tatizo la ukosefu wa vituo rasmi vya daladala linawatesa wananchi na watumiaji wa barabara kwa ujumla.

(a) Je, ni lini Serikali itajenga kituo rasmi cha daladala katika eneo la mjini na kuliacha eneo la Michenzani tobo la pili liwe lenye kuvutia na kuondoa kero zilizopo hivi sasa.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo rasmi vya daladala katika maeneo mbali mbali ya mji wetu, ili kuondosha usumbufu kwa abiria na watumiaji wa barabara.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

132. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa suala la usalama wa afya za wananchi ni jambo muhimu sana linalohitaji kulindwa kwa umuhimu wake. Na kwa kuwa hali ya usalama wa afya za wananchi wa Wesha na vitongoji vyake katika Wilaya ya Chake – Chake umo hatarini kutokana na kuwepo kwa hali mbaya ya bohari ya mafuta (poor deport infrastructure), kutokana na matangi yake kuvuja na kuchakaa kwa muda mrefu sana.

(a) Je, Serikali yetu ya awamu ya nane inalifahamu hili.

(b) Ni hatua gani za kimkakati zimechukuliwa ili kukabiliana na tatizo hili.

(c) Kwa kuwa muda mrefu umepita bila ya matangi haya kubadilishwa, Je, Serikali haioni kuwa ipo haja kituo kile kurasimishwa na kupewa wawekezaji kwa lengo la kukiendeleza ili kulinda usalama wa wananchi.

178. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali katika jitihada zake za kudhibiti kupotea kwa mapato ya kodi ilipiga marufuku maduka ya kubadilishia fedha (bureau de change) zilizokuwa zikienea bila ya kufuata utaratibu.

(a) Je, Serikali inatambua kuwa maduka hayo yapo na yanazidi kuongezeka hali inayopelekea Serikali kukosa fedha nyingi.

(b) Kuna sababu zipi za msingi zinazopelekea kuongezeka kwa maduka hayo pamoja na watu binafsi wanaofanya shughuli hizo licha ya marukufu ya Serikali na uwepo wa vyombo vya udhibiti.

(c) Ni ipi kauli ya Serikali kuhusu kadhia hiyo.

**<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>**

173. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kitengo cha usulihishaji (Dispute Handling Resolution Unit “DHU”) kinasaidia sana kuamua migogoro ya wafanyakazi na waajiiri.

(a) Je, kwa nini migogoro inachelewa kuamuliwa na mara nyengine inachukuwa zaidi ya miezi sita.

(b) Je, Wizara haioni kuwa inapelekea wafanyakazi kukosa haki zao pindi kesi zikienda Mahakamani na kucheleweshа kutolewa hukumu.

(c) Ni sababu zipi zinazopelekea maamuzi ya kitengo “DHU” kutotekelezwa au kuchelewa.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

17. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Zanzibar ina utamaduni wake ambao uwepo wake ni sehemu moja ya vivutio kwa wageni wetu wanaokuja kutalii hapa kwetu.

Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kuendeleza mchezo wa ng’ombe pamoja na michezo mengine ya asili.

22. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Katika eneo la Kishindeni Shehia ya Mapofu Jimbo la Wingwi, kuna uwanja wa mchezo wa mpira wa miguu uliojengwa na Serikali ya SMZ hivi miaka ya karibuni. Uwanja huo umekuwa kivutio kikubwa kwa vijana wetu katika kufanyia mazoezi na kukuza vipaji vyao.

(a) Je, ni gharama gani zilizotumika katika ujenzi wa kiwanja hiki.

(b) Kwa vile eneo hili la Kishindeni ni kubwa na halitumiki kwa matumizi ya makaazi wala kilimo. Je, Wizara ina mpango gani katika kuliendeleza eneo lile na kuwa sehemu ya kijiji cha michezo kwa upande wa Pemba.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

235. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango wa kusambaza umeme vijijini na kuwapelekea wananchi wa vijiji hivyo, nguzo na transforma bila ya malipo.

Je, ni lini utafikishwa umeme katika vijiji vya Simaovu, Kiwarani na vyengine katika jimbo la Bumbwini.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

2. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kupeleka maendeleo kwa wananchi katika Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kujenga barabara zenye kiwango cha lami, kuanzia Wete mjini hadi Konde, sambamba na Wete mjini hadi Gando. Katika kufanikisha miradi hii, Serikali ilifanya uharibifu wa majengo pamoja na mazao ya wananchi ambayo mengine hadi leo hii bado hayajalipwa fidia.

Je, ni lini Serikali itamalizia malipo kwa wale ambao hadi leo majengo pamoja na mazao yao hayajalipwa fidia.

3. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege kisiwani Pemba hutoza shilingi elfu moja kwa kila gari inayoingia uwanjani, kama tozo la maegesho (Parking fee), na kwa kuwa gari za kawaida zimetengewa maegesho yenye kiwango cha vumbi kiasi ambacho gari nyingi hupoteza rangi zake za asili na hatimae kukosa wateja kwa zile gari za TAXI.

Je, ni lini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itajenga maegesho ya kisasa yenye kiwango bora katika uwanja wa ndege wa Pemba.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

65. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar tayari imepokea maombi ya mkopo kwa waombaji wa mwaka wa masomo 2021/2022. Hata hivyo, wanafunzi wengi hawakuweza kupata fursa ya kuomba mkopo huo kutokana na vigezo vya kutomaliza masomo yao na hata baada ya kumaliza masomo ilikuwa tayari maombi yameshafungwa.

Je, Bodi imeandaa mpango gani wa kuwasaidia wanafunzi wa aina hiyo.

114. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naendelea kuipongeza Serikali yetu kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuimarisha elimu Zanzibar, ikiwa ni pamoja na kujenga majengo mbali mbali ya skuli za msingi na sekondari. Pamoja na jitihada hizo, kuna baadhi ya skuli zinakabiliwa na tatizo la kuvuja, ikiwemo skuli ya Shungi.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu vipi tatizo la kuvuja kwa skuli ya Shungi.

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kuondosha tatizo la kuvuja kwa skuli ya Shungi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

42. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Maendeleo ya Mifugo hapa Zanzibar ndiyo yenye jukumu la kufuatilia mwenendo wa magonjwa ya mifugo, kuwakinga na kuwatibu wanyama mbali mbali pale wanapoathirika na maradhi. Hivi karibuni ndani ya mwezi wa Agosti, 2021 vyombo vya habari viliripoti tishio la kuwepo mbwa walioaminika kuugua ugonjwa wa kichaa na kushambulia wakaazi wa Kiembesamaki na maeneo mengine.

(a) Je, Wizara inayo taarifa juu ya kuwepo kwa hali hiyo.

(b) Je, ni hatua gani za haraka zimechukuliwa katika kuwafanya wananchi waishi bila tishio lolote dhidi ya maisha yao.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

32. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Wazee wamefarijika sana na ruzuku inayotolewa na Serikali kwa wenye umri wa miaka 70 na zaidi. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wazee wenye umri wa miaka kasoro ya 70 ambao hawana uwezo kimaisha.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuangalia zaidi wazee wenye shida na wanaostahiki msaada na sio tu wazee wa miaka 70 ambao kuna wengi ambao hawana shida za kustahiki kusaidiwa na Serikali.

(b) Je, Serikali haioni kwamba wengi wa wazee wenye shida za kweli hufariki kabla hawajafikia umri wa miaka 70.

211. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Wananchi wa jimbo la Mkwajuni wanategemea kwa kiasi kikubwa kupata huduma za afya katika hospitali ya Gamba, lakini hospitali hiyo ni mbovu na sio rafiki kwa kuwahudumia wagonjwa.

(a) Je, ni lini Serikali itaifanyiwa matengenezo makubwa hospitali hiyo ili iwe ya kisasa zaidi.

(b) Je, ni lini ukuta unaoizunguka hospitali hiyo utafanyiwa matengenezo.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka mlinzi katika eneo hilo ili kuwa usalama wa uhakika.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

203. MHESHIMIWA SHADYA MOH’D SULEIMAN (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kumekuwa na hali ngumu ya maisha hivi sasa ambayo inasababishwa na baadhi ya wafanyabiashara kupandisha bei za bidhaa za ujenzi na vyakula.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi kwa wafanyabiashara hao ili kunusuru maisha ya wananchi.

(b) Je, Serikali haioni kwa sasa wakati umefika wa biashara kuendeshwa na Serikali licha ya kuwa ni biashara huria.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

118. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika juhudi za kuibadilisha Zanzibar kiuchumi na kimaendeleo, Serikali ya Awamu ya Nane imekuja na kauli mbiu ya uchumi wa buluu na kuchukua juhudi kubwa kuuimarisha uchumi huo. Hata hivyo, kuna maeneo mengi hayajapangwa vizuri na kuzifanya juhudi za Serikali kukwazwa na changamoto mbali mbali, wakati kuna kampuni nyingi nchini zenye uwezo wa kuisaidia Serikali katika suala zima la uchumi wa buluu.

Je, Serikali iko tayari vipi kuitumia Kampuni ya Kizalendo ya "Property International Co. Limited', katika kuimarisha uchumi wa buluu nchini.

218. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika kikao kilichopita Mheshimiwa Waziri alitoa ahadi ya kuwatembelea wakulima wa mwani wa jimbo la Mkwajuni pamoja na kuwapelekea mbegu mpya za zao la mwani.

(a) Je, ni lini Serikali itatoa mbegu mpya ya mwani, ili wananchi waweze kunufaika na ukulima wa zao hilo.

(b) Je, ni wapi Serikali imejenga kiwanda kipya cha zao la mwani.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

64. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Pamoja na juhudi za Serikali kuhamasisha utalii na ujenzi wa hoteli katika maeneo mbali mbali, kumekuwa na malalamiko mengi ya wananchi wanaotumia njia za karibu na mahoteli kufanyia shughuli zao za kibinadamu ikiwa ni pamoja na kuelekea kondeni na pwani.

(a) Je, Serikali inaitambua kadhia hii.

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa wawekezaji hao.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Kazi, Majukumu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Zanzibar,**
**24 Disemba, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**